# JARIDA LA VIWANDA NA UWEKEZAJI

TOLEO LA MWAKA 2024-2025

## FURSA MBALIMBALI ZA UWEKEZAJI SINGIDA



Eneo hili lipo Utemini lenye Block 3 plot 62 lenye Na.1172101 na ukubwa......Uk10



Uwepo wa mabwawa/maziwa yenye viumbe mbalimbali.....uk20




Katika tarafa ya mgori kuna msitu wenye ukubwa wa zaidi ya hekta 40,000/= ambao unafaa kwenye ufugaji wa nyuki bila.....uk19









Kilimo cha kitunguu kwa kutumia mradi wa umwagiliaji... uk,16



SINGIDA






Misitu hutoa fursa ya kiuchumi kwa watu na mashirika kupitia mikopo.....uk,16









Kutokana na uwepo wa mabwawa/maziwa sita kuna fursa..uk,19



Mkuu wa Mkoa wa Singida
Mhe. Halima Dendego



Katibu Tawala Mkoa wa Singida
Dkt. Fatuma Mganga



Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Viwanda
Donatila Vedasto

# Yaliyomo ndani ya Jarida

1: Utangulizi.uk4

2: Hali ya uwekezaji katika mkoa.uk5

3: Maboresho ya Miundombinu katika Mkoa. uk7

4: Halimashauri ya Wilaya ya Mkalama.uk8

5: Maeneo yanayomilikiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.uk10

6:Maeneo ya Uwekezaji Wilaya ya Manyoni.uk13

7: Maeneo ya Uwekezaji Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.uk17

8:Ofisi zinazotoa huduma za uwekezaji kwa mda mfupi.uk18

9:Fursa mbalimbali kama zilivyoainishwa.uk19

10:Picha mbalimbali zikionyesha matukio na fursa katika mkoa. uk21

# UTANGULIZI

Serikali inatambua kwamba ukuaji wa Uchumi katika nchi yetu unategemea sana uimara wa sekta binafsi, Sekta binafsi iliyo imara hutoa ajira, huongeza kipato cha wananachi, huwezesha serikali kukusanya kodi, hupunguza umasikini, huwezesha ustawi wa jamii na kufanya Uchumi kuendelea kukua.

Ili Sekta binafsi iweze kufanya yote hayo inahitaji mazingira bora ya kufanyia biashara na uwekezaji na jukwaa kwa ajili ya sekta binafsi kutoa Mawazo yake katika kuandaa na kutekeleza mipango na sera nyingine za serikali.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, serikali ilianzisha Baraza la Taifa la Biashara kupitia waraka wa Rais Na.1 wa 2001 na kutangazwa kwenye gazeti namba 39 la 28 septemba 2001 kama jukwaa rasmi la majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binasfi. Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya yalianzishwa mwaka 2005 na 2008

Majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kuptita Mabaraza ya Biashara yanalenga kujenga uelewa wa Pamoja kuhusu masuala mbalimbali ya kimkakati ya kuboresha mazingira ya biashara nakuainisha namna bora ya kutumia fursa mbalimbaliza kiuchumi zilizopo sambamba na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

## Mabaraza haya yana faida mbalimbali ikiwa ni Pamoja na

1.Kuwezesha uchambuzi wa kina wa changamoto za mazingira ya biashara na kupendekeza maboresho ya mazingira ya biashara, mfano sheria mpya, marekebisho ya sheria zilizopo na kuhuisha taratibu katika mamlaka mbalimbali na kuanzisha kwa taasisi mpya.

2. kujenga mazingira ya uaminifu, uelewa na ushirikiano kati ya sekta za umma na sekta binafsi, endapo serikali na Sekta binafsi hazitakuwa na mahusiano mazuri na hakuna majadiliano kati yao, wawekezaji hupoteza Imani na ujasari wa kuwekeza.

3. Kurahisisha utekelezaji wa maboresho ya kisera, Sekta Binafsi ikitambua lengo la serikali, ni rahisi kuunga mkono utekelezaji wa mpingo na sera mbalimbali ya mipango ya serikali.



## HALI YA BIASHARA NA UWEKEZAJI

Mkoa wa Singida umejipambanua kama sehemu yenye rasilimali nyingi ambazo zinaweza kuendelezwa kupitia Viwanda, Biashara na Uwekezaji wa aina mbalimbali. Hivyo, tukiwa na ushirikiano wa karibu kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi tuna imani kwamba Mkoautaendelea kufunguka na kukuza Biashara na Viwanda vya kisasa ambavyo vitaongeza ajira na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa Mkoa wetu na Nchi kwa ujumla. Aidha, Mkoa unaendelea kusimamia Sheria, kanuni na taratibu za Biashara,Viwanda na uwekezaji na kuhakisha zinazingatiwa na kusimamiwa katika Sekta hii.

Mkoa una jumla ya Wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo wapatao 10,593 ambao wamesajiliwa na Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) na kupewa namba ya utambulisho ya mlipa kodi (TIN) na wamerasimishabiashara zao

, pia hufanya biashara hizo kwa kufuata sheria kanuni na taratibu zilizowekwa na serikalina wanavibali vya kufanyiaBiashara zaozikiwemo Leseni za Biashara.

Mkoa unaendelea na zoezi la kuwatambua wafanyabiashara ambao hawajarasimisha biashara zao ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu juu ya kurasimisha biashara, jinsi ya kupata mikopo kutoka taasisi za fedha, ufungashaji wa bidhaa, namna ya kukuza biashara, kupata masoko, namna ya kupata nembo ili ziwasaidie kutangaza biashara na kukuza masoko ya bidhaa zao.

Aidha, Mkoa una jumla ya wafanyabiashara wa biashara ndogondogo wapatao 5,800 ambao hawako kwenye mfumo rasmi,Elimu inaendelea kutolewa kwa wafanyabiashara hao ili warasimishwe kupitia vitambulisho vya Wafanyabiashara ndogondogo ambavyo vinaratibiwa na wizara ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake na makundi maalumu. Hata hivyo, zoezi la kuhakiki takwimu za wafanyabishara hao linaendelea katika Halmshauri za Mkoa wa Singida kupitia





## HALI YA VIWANDA







Mkoa unaendelea kuhudumia Viwanda vilivyopo na kusimamia uanzishwaji wa Viwanda vipya. Hadi kufikia Desemba,2024 Mkoa ulikuwa na Jumla ya Viwanda vinavyofanya kazi 1,954 kati ya hivyo Viwanda Vikubwa ni 9, Viwanda vya kati 11, Viwanda vidogo 420 na Viwanda vidogo sana ni 1,516. Viwanda vidogo na vya kati vinaendelea kusimamiwa kwa karibu ili viweze kutoka kwenye sifa yake ya sasa na kuwa vikubwa.


Aidha, licha ya maendeleo ya viwanda kuwa mazuribado kuna changamotoya upatikanaji wa malighafi za kutosha hasa kipindi ambacho si cha msimu wa kilimo inayopelekewa na ukosefu wa mitaji ya kutosha kwa baadhi ya wamiliki wa Viwanda Pamoja na kutokuzalisha kwa wingi Malighafi hizo. Hata hivyo, Mkoa unaendelea kusimamia uzalishaji wa mazao kwa tija na kuboresha mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa watoa huduma za kifedha na Viwanda ili viweze kuzalisha kipindi chote cha mwaka, pia wawekezaji wa viwanda wameendelea kutembelewa na kupewa elimu ya kuanzisha mashambaya kilimo cha kisasa cha umwagiliaji ambacho kinaweza kuwa suluhu ya ukosefu wa malighafi hususani katika Mbegu za Alizeti.

Ikumbukwe kuwa,Dhamira ya serikali ni kuthibiti mafuta ya kula kutoka nje ya Nchi, Singida ni moja ya Mkoa unaotegemewa kuzalisha mafuta mengi, hivyo hatuna budi kupambana na tatizo la ukosefu wa malighafi ili tuweze kutatua changamoto hii.

## HALI YA UWEKEZAJI KATIKA MKOA

Hadi Desemba, 2024, Mkoa ulikuwa na Jumla ya wawekezaji 40 kati ya hao wakubwa ni 29 na wa kati 11, Wawekezaji hao wamewekeza katika viwanda vya mazao mbalimbali yanayolimwa Mkoa wa Singida, Hoteli za kawaida (zisizo za Kitalii), Nyumba za kulala wageni, Apertments, Kumbi na michezo ya watoto. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa bado kuna uhitaji wa uwekezaji mkubwa katika Mkoa wa Singida.

Hata hivyo, katika Mwongozo wa Uwekezaji ulioandaliwa na Mkoa na kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 ambapo Mkoa una jumla ya watu takribani Milioni mbili na elfu nane na Hamsini na nane (2,008,058), Mwongozoumebainisha fursa mbalimbali za uwekezaji katika Sekta mbalimbali ambazo ni Ujenzi wa Hoteli za Kitalii, Ujenzi wa Kumbi za kisasa zaMikutano ya kitaifa naKimataifa, ujenzi wa sehemu za kupumzikia, viwanja vya michezo ya Watoto, Shopping mall, soko la vitunguu la kimataifa, shule binafsi(Sekondari na Msingi),Vyuo vya ufundi, Viwanda vya (kusindika mazao mbalimbali ya kilimo, mazao ya mifugo, Saruji, Vifungashio, Vifaa vya ujenzi na Madini), Mashamba ya kisasa ya umwagiliaji



kuweka mikakati mbalimbali ya kuvutia wawekezaji kutokana na vivutio na fursa zilizopo katika Mkoa wa Singida, Mikakati hii ni Pamoja na:

- o Kutenga maeneo ya uwekezaji ambapo kila Halmashauri Imetenga maeneo hayo yenye ukubwa tofautitofauti.
- o Kuboresha miundombinu na huduma mbalimbali kama vile barabara, umeme na maji na hivi karibuni ujenzi wa Treni ya mwendo kasi unatarajia kufika katika Mkoa wa Singida.
- o Kutangaza vivutio vya uwekezaji vilivyopo katika Mkoa, ambapo mkoa ulifanya jukwaa la uwekezaji mwezi septemba, 2024 ili kutangaza vivutio hivyo ndani na nje ya nchi.
- o Kusambaza Vipeperushi vya fursa za uwekezaji katika Maonyesho ya Kitaifa yaya wakulima Nane nane yaliyofanyika Mkoani Dodoma mwezi Agosti,2024.
- o Kutembelea Wawekezaji waliopo Mkoa wa Singida na kuwapatia taarifa za fursa hizo na Mwekezaji mmoja ameonyesha nia ya kuwekeza katika ujenzi washopping mall.
- o Mkoa umeelekeza Halmashauri zote za Mkoa wa Singida kuhakikisha wanawekeza katika vitega uchumi mbalimbali kulingana na jiografia ya maeneo yao.
- o Mkoa umeandaa fursa za uwekezaji zilizopo na kuziweka kwenye tovuti ya Mkoa na kwenye Mwongozo wa Fursa za uwekezaji wa Mkoa ili wawekezaji wenye nia ya kuwekeza waweze kuzifahamu.

# MABORESHO YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA KATIKA MKOA

Mkoa umeendelea kuboresha Miundo mbinu na huduma katika maeneo mbalimbali ya mkoa, miundo mbinu hiyo imeboreshwa na Sekta ya Umma pamoja na SektaBinafsi, Aidha, baadhi ya maboresho ya miundo mbinu hiyo yameanishwa kwa kila

## MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZILIZOBORESHWA NA SEKTA YA UMMA.

Serikali imeboreshwa miundo mbinu mbalimbali ili kuweka mazingira ya biashara na uwekezaji vizuri, Miundo mbinu hii imepelekea kuongezeka kwa wawekezaji na kusababisha Mkoa wa Singida kuendelea kukua kwa Kasi zaidi. Baadhi ya Miundo mbinu iliyoboresha na Sekta ya Umma ni kama ifuatavyo:

Ujenzi wa Kituo cha Biashara (One Business Stop Centre katika Halmashauri ya Manispaa, Kituo hicho kilijengwa ili kurahisisha utoaji wa hudama kwa wawekezaji na wafanyabishara kwa ujumla, kituo hiki kinaendelea kutoa huduma hizo kwa Wafanyabiashara.






Ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji mashambani kwa ajili ya kuongeza eneo la umwagiliaji ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya mpunga na mbogamboga katika Wilaya.

Maboresho ya ujenzi wa uzio wa mifugopamoja na ujenzi wa vyoo kwaajili ya wafanya biashara kupata huduma katika mnada wa Itigi mjini uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.









Mkoa wa Singida kupitia TARURA katika jitihada za kukwamua wananchi kutoka kwenye vikwazo vinavyohusu mawasiliano kwa njia ya Barabara na kuweka vivuko katika maeneo ya vijijini na mijini, imefanikiwa kuboresha miundombinu mbalimbali ambapo baadhi yake ni kuongeza mtandao wa barabara zinazopitika kwa vipindi vya changamoto ya mvua, na hivyo kuchangia (indirect) kwenye pato la taifa kwa kuwezesha biashara za mazao ya biashara na chakula kuweza kufika kwenye masoko kwa uharaka bila kuharibika, na hivyo kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao na kuwasaidia wawekezaji na wafanyabiashara kwa Ujumla. Baadhi Picha za maboresho ya miundombinu hiyo ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini:






## HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI

| Na | Picha kabla ya Matengenezo kuanza | Picha baada ya Miradi kukamilika |
|---|---|---|
| 1. | <br>MINYUGHE KATIKA BARABARA YA MTAMAA – MINYUGHE – MTAVIRA | <br>MINYUGHE KATIKA BARABARA YA MTAMAA – MINYUGHE – MTAVIRA |
| 2. | <br>BOKSI KALAVATI KATIKA BARABARA YA MISUGHAA – MSULE – SAMBARU | <br>BOKSI KALAVATI KATIKA BARABARA YA MISUGHAA – MSULE – SAMBARU |

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

| Na. | Picha kabla ya Matengenezo kuanza | Picha baada ya Miradi kukamilika |
|---|---|---|
| 1. | <br>Ujenzi wa kalavati barabara ya Manyoni-Mbwasa-Kamenyanga | <br>Kalavati barabara ya Manyoni-Mbwasa-Kamenyanga |
| 2. | <br>Ujenzi wa barabara ya Sasilo – Imalampaka | <br>Barabara ya Sasilo – Imalampaka |

## HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

| Picha kabla ya Matengenezo kuanza | Picha baada ya Miradi kukamilika |
|---|---|
| <br>Ujenzi wa barabara ya Itigi – Damwelu – Mgamboo | <br>Barabara ya Itigi – Damwelu – Mgamboo |

## HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | <br>Ujenzi wa Barabara ya mjini Ilongero kwa kiwango cha lami (Double Surface Dressing) | <br>Barabara ya mjini Ilongero kwa kiwango cha lami (Double Surface Dressing) |

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA




a ya Unyamikumbi bonde la Shule ya Upili Unyamikumbi wa

Barabara ya Unyamikumbi bonde la Shule ya U Unyamikumbi

| Na. | Picha kabla ya Matengenezo kuanza | Picha baada ya Mradi kukamilika |
|---|---|---|
| 1. |  Mwonekano wa barabara ya Mwangeza-kipamba kabla ya matengenezo |  Mwonwkano wa daraja katika barabara ya Mwangeza-Ki baada ya matengenezo |

## HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA

| | | |
|---|---|---|
| 1. |  Picha Na.1 : Mwonekano wa barabara ya Mwanza (Kiomboi Mjini) kabla ya ujenzi kwa kiwango cha lami |  Picha Na.2 : Mwonekano Barabara ya Mwanza(Kiomboi Mjini) baadaya ujenzi kwa kiwango cha lami |
| 1. |  Picha Na.3 : Mwonekano wa mto Kinkungu barabara ya Shelui – Mtoa – Ndago kabla ya kuanza ujenzi wa kalavati la zege |  Picha Na.4 : Ujenzi wa Kalavati la zege Mto Kinkungu barabara ya Shelui – Mtoa – Ndago |

## MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZILIZOBORESHWA NA SEKTA BINAFSI

Kiwanda cha Mafuta cha Mount Meru Millers ltd kinaendelea kutoa huduma ya chakula kwa wanafunzi wote 1314 wa shule ya Msingi Manguanjuki kama picha zinavyoonyesha hapa chini:




Kiwanda cha Wild flower grain & Oil Mills co.ltd kimeboresha miundombinu ya ujenzi wa Visima vya maji vitatu, ambavyo vinatoa huduma yamaji kwa wananchi wanaozunguka eneo la kiwanda KatayaMandewa eneo la Njuki. Picha ya visima hivyo ni kama inavyonekena hapa chini:






Mgodi wa Uchimbaji madini SHANTA uliopo Ikungi kata imeboresha miundo mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Msingi ya Mbogo iliyopo katika Kijiji cha Tupendane,Uendelezaji wa Ujenzi wa Stendi mpya kata ya Unyahati na ununuzi wa Trekta na trela yake kwa ajili ya kusomba taka ngumu makao makuu ya Halmashauri na Ujenzi wa Wodi katika Kijiji cha Mang'onyi.Picha zimeambatishwa hapa chini:
















## KIWANDA CHA BIOSUSTAIN TANZANIA LTD

Kiliboresha Miundombinu kwa kujenga Bweni la Wasichana lenye uweze wa kuhudumia wasichana 80 waliokuwa wakabaliwa na changamoto ya kutembea umbali mrefu takribani km. 20 na kuweka vitanda 40, pia walichimba Kisima cha Maji na kuweka Tenki la maji lenye ujazo wa lita 10,000 ili kuhakikisha upatikanaji wa maji katika Shule ya Sekondari ya Mtekente iliyopo Kata ya Mtekente Wilaya ya Iramba. Picha zimeambatishwa hapo chini:







# MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA UWEKEZAJI

Maeneo yanayomilikiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni kama yalivyoanishwa hapo chini

## 1. ENEO LA SEMA

Eneo hili lipo Utemini lenyepande (Block) 3 kiwanja Na. 62 lina ukubwa wa mita za Mraba 21,610, eneo limepimwa na lina Hati na matumizi yake ni kwa ajili ya uwekezaji wa Viwanda na Biashara.



## 2. ENEO LA SIDO

Eneo hili lipo Utemini kwenye pande (block) 3 na kiwanja Na. 60 na lina ukubwa wa mita za Mraba 5,107, eneo hili limepimwa na lina Hati na matumizi yake ni kwa ajili ya uwekezaji katika Viwanda na Biashara.



## 3. ENEO LA JENGO LA UTAMADUNI

Eneo hili lipo Ipembe karibu na jengo la Benki ya NMBpande (Block) A na kiwanja Na. 4 lina ukubwa wa mita za Mraba 2,957 na matumizi yake ni kwa ajili ya majengo ya Ofisi.



## 4. JENGO LA NMB

Lipo Ipembe, pande (Block) A, kiwanja Na. 3, ukubwa wa mita za mraba 2,401 na matumizi yake ni kwa ajili ya Ofisi.





## 5. Uwanja wa Maonesho Mandewa – Kata ya Mandewa, eneo halijapimwa









## MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA UWEKEZAJI

1. Eneo la stendi ya zamani lenye ukubwa wa - 10,989.7 sqm



2. Mashamba ya kufuga Nyuki - 499 Hekta – Kata ya Kisaki



3. Nyumba za kuishi na kupangisha (Apartments), jengo la biashara - 750 sqm



4. Ufukwe wa wazi Kindai & Singidani - 20 Hekta



**MAENEO YA UWEKEZAJI YALIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI.**

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imetenga maeneo ya uwekezaji mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini:

| NA. | FURSA ZA UWEKEZAJI | ENEO | UKUBWA |
|---|---|---|---|
| 1. | Uzalishaji wa Umeme kwa kutumia upepo | Mkwese | Ekari 160.4 |
| 2. | Kilimo cha korosho na AlizetiMasigati | | Ekari 2000 |
| 3. | Eneo la kuwekeza Viwanda mbalimbali | Mnadani njia ya Kwenda ChikolaEkari | 115.6 |
| 4. | Eneo la uchimbaji wa chumvi Kinangali | | Ekari 50 |
| 5. | Eneo la uchimbaji wa madini ya dhahabu | -Makulu-Londoni<br>-Isseke-Mafurungu | |
| 6. | Eneo la ujenzi wa Hospitali | Setelaiti | Ekari 11.5 |
| 7. | Eneo la ujenzi wa shule | Setelaiti | Ekari 6.6 |
| 8. | Eneo la stendi ya mabasi | Manyoni mjini | |
| 9. | Eneo la ufugaji Mifugo | Mkwese | Ekari 11,860 |
| 10. | Eneo la uwanja wa Mpira | Manyoni mnadani | Ekari 5 |

1. Eneo kwaajili ya kilimo cha korosho na Alizeti – Masigati Ekari 2,000



2. Eneo la ufugaji Mifugo – Mkwese Ekari 11,860



3. Eneo kwaajili ya Ujenzi wa Shule na Hospitali – Satelaiti Ekari 18.1



4. Eneo kwaajili ya ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Manyoni Mjini



5. Eneo kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa mpira – Manyoni mnadani Ekari 5





## MAENEO YA UWEKEZAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA.


### 1.ENEO LILILOPO IPEMBE MKABALA NA KITUO CHA POLISI CENTRAL

Eneo la Central Police ipembe lenye ukubwa wa mita za mraba 9,517. Eneo linafaa kwa shughuli kama ujenzi wa vibanda vya biashara, kumbi za mikutano, super markets na vituo vya mafuta.









## 2. ENEO LENYE NYUMBA ILIYOKUWA YA MKURUGENZI

Eneo la Bomani Unyakumi, Lenye ukubwa wa mita za mraba 5,603. Eneo linafaa kwa shughuli kama ujenzi wa hoteli za kisasa.



## 3. ENEO LA UTEMINI SIDO

NyumbaNamba SDC/HQ/ADMN/RB/13, SDC/HQ/ADMN/RB/14, SDC/HQ/ADMN/RB/15 na SDC/HQ/ADMN/RB/16. Nyumba hizi zipo karibu na Ofisi ya SIDO Mkoa, Nyumba zipo kwenye eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 1,020, zinafaa kwa shughuli zifuatazo, viwanda na warehouse



## 4. 332 KITALU X UTEMINI

Kiwanja hiki chenye ukubwa wa mita za mraba 900 kilitengwa kwa ajili ya matumizi ya ujenzi wa ghala (Godown), kiwanja hiki ni kitupu (hakijaendelezwa)



# MAENEO YA UWEKEZAJI YALIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA

1. Kilimo cha vitunguu katika kijiji cha Msingi



2. Kilimo cha Alizeti



3. Biashara ya hewa ya ukaa kwenye misitu yenye ukubwa wa Heka 3,623




4. alighafi ya mawe kwaajili ya ujenzi wa kiwanda cha



## MAENEO YA UWEKEZAJI YALIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA

1. Uvunaji na uuzaji wa Hewa ya ukaa, uchimbaji wa madini na utalii (waterfalls, historical sites na sehemu za kujenga hoteli) – Ha 30,365



2. Uvuvi, Utalii (fukwe za kujenga hoteli), ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba na kujenga mabwawa ya pembeni kufugia samaki – Km za mraba 105



3. Ujenzi wa Taasisi na viwanda – Zaidi ya Ekari 100



4. Kilimo cha umwagiliaji, utalii na mafunzo ya kilimo - Eneo la bwawa Ha 65 na kidakio cha maji (catchment area) Ha 12,000







## MAENEO YA UWEKEZAJI YALIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

1. Hotel site pande (Block) E –Bangayega 2,688 Sqm



2. Shopping mall (maduka makubwa) pande (Block) X - Kata ya majengo 5,724 Sqm



3. Uwekezaji wa Machinga complex (informal Trading activities) pande (Block) X - Kata ya Majengo 18,583 Sqm



4. Service industry (eneo la viwanda) pande (Block) E – Bangayega 39,660 Sqm



5.Uwekezaji wa Soko pande (Block) E – Bangayega 5,609 Sqm





## KARIBU UWEKEZE NDANI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA.

ofisi ya mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya singida kupitia idara husika kama idara ya viwanda biashara na uwekezaji, idara ya miundombinu, idara ya kilimo na mifugo na idara nyingine inatoa usaidizi wa haraka kwenye kufanikisha uwekezaji wa aina yoyote

# OFISI HIZI ZITATOA VITU VIFUATAVYO NDANI YA MUDA MFUPI.

- VIBALI VYA UJENZI
- MSAADA WA UPIMAJI WA MAENEO NA HATI
- MAPENDEKEZO YA MAENEO MUHIMU YA KU FANYA UWEKEZAJI
- LESENI ZA BIASHARA NA VIBALI VINGINE
- KUSAIDIA UPATIKANAJI WA MASOKO.

## Zifuatazo ni baadhi ya fursa ambazo zimeainishwa

### 1.USINDIKAJI WA MAZAO YA MIFUGO.

Usindikaji wa mazao ya mifugo kama ngozi, nyama, kwato, manyoya, maziwa na mayai ni fursa ambayo haijaanza kufanyiwa kazi kwa ukamilifu katika halmashauri ya wilaya ya singida kutokana na uwepo wa idadi kubwa ya mifugo kama inavyoonesh-wa kwenye jedwali.

| s/n | Mnyama/ndege | idadi |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 166,990 |
| 2 | mbuzi | 72,880 |
| 3 | kondoo | 41,002 |
| 4 | kuku | 645,414 |
| 5 | kanga | 8407 |
| 6 | bata | 4371 |
| 7 | njiwa | 8939 |
| 8 | sungura | 4250 |
| | JUMLA | 948,003 |



### 2. FURSA YA UFUGAJI SAMAKI.

Kutokana na uwepo wa mabwawa/maziwa sita kuna fursa ya ufugaji samaki na uvu-naji wa samaki kwenye mabwawa haya ambayo yanapatikana kwenye kata zifuatazo

1. Ikhanoda
2. Ilongero
3. Makuro
4. Mwasauya
5. Mgori
6. Msange
7. Kinyeto
8. Mrama.



Samaki wanaoweza kupandwa kwenye mabwawa haya ni kambale, sato, na perege.

### 3. FURSA YA USINDIKAJI UNGA WA MAHINDI NA KUFUNGASHA PAMOJA NA KUONGEZA VIRUTUBISHO.



Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zaidi ya gunia 825,000 zilisafirishwa kwenda maeneo mbalimbali kutoka ndani ya hal-mashauri ya wilaya ya singida, kutokana na uzalishaji huu wa mahindi ni wazi ka-bisa kuwa vinahitajika viwanda kwaajili ya kusindika mahindi hayo, kufungasha na kuongeza virutubisho kwenye unga(-fortification)





Katika halmashauri yenye kata 21 na vijiji 84 hakuna hata kiwanda kimoja kinachosindika mahindi na kufung-sha pamoja na kuongeza virutubisho

- Soko la ndani na nje la unga ni kubwa.
- Umeme kwaajili ya viwanda upo.
- Maji
- Barabara
- Maeneo ya kuwekeza/kujenga

### 4. FURSA YA UFUGAJI NYUKI NA USINDIKAJI WA MAZAO.






Katika tarafa ya mgori kuna msi-tu wenye ukubwa wa zaidi ya hekta 40,000/= ambao unafaa kwenye ufugji wa nyuki bila kuathiri ustawi wa msitu huo, uwekezaji kwenye ufugaji nyuki ukifanyika kitaalamu na kwa kiwango kikubwa unaweza kuifanya singida kuwa kitovu cha asali kama mkoa wa tabora, ufugaji huo wa nyuki utaenda sambamba na usindikaji wa mazao ya nyuki(viwan-da vya usindikaji) kama asali.



## 5. FURSA YA UTALII WA NDANI.



Ndani ya halmashauri ya wilaya ya singida kuna vivutio mbalimbali vya utalii ambavyo vinaweza kuboreshewa mazingira na kuweza kusaidia kuongeza pato la halmashauri na mwananchi mmoja mmoja. Vivutio hivyo ni kama ifuatavyo;

- Uwepo wa mabwawa/maziwa yenye viumbe mbalimbali kama ndege wazuri, vyura, samaki wa aina mbalimbali pamoja na mitumbwi/ngalawa za asili.
- Msitu wa mgori ambao ndani yakekuna miti ya asili, vichaka vya asili.
- Uwepo wa vitu vya asili kama ngoma za kitamaduni na vyakula vya kitamaduni.
- Uwepo eneo lenye upepo mkali unaoweza kuzalisha umeme.
- Uwepo wa eneo katika njiapanda ya merya ambapo unaweza kuona vizuri mawio na machweo ya jua.

## 6. FURSA KWENYE ELIMU, AFYA NA MICHEZO.

Ndani ya halmashauri ya wilaya ya singida hakuna chuo kikuu, chuo cha ufundi, viwanja vya kisasa vya michezo, maduka makubwa ya madawa(pharmacy) maabara za kisasa na maduka ya vifaa vya michezo. Maeneo kwaajili ya uwekezaji wa aina hiyo yapo kwa mfano eneo lililotengwa njiapanda ya merya kwaajili ya viwanja vya michezo lipo wazi.



## 7. FURSA KATIKA KILIMO CHA UMWAGILIAJI.



tambo ya kilimo kutokana na maeneo hayo kuwa na tambalale, pia maeneo hayo yana rutuba na yanafaa kwa kilimo cha mazao ya aina tofauti kama miwa, mahindi, maharage, vitunguu, alizeti, dengu, mbaazi, mpunga, korosho n.k. Kilimo kisichotegemea mvua ni kilimo ambacho kimejidhihirisha kuwa ni kilimo cha uhakika.


mahitaji ya soko, maeneo yaliyopo halmashauri ya wilaya ya singida yanaruhusu kilimo cha umwagiliaji, maji yanapatikana kutoka kwenye uchimbaji wa visima na kutumia mashine za kuvuta na kusambaza maji, aidha serikali imeanza kujenga miundombinu ya umwagiliaji ambayo itarahisisha uwekezaji kwenye kilimo.

## 8.FURSA KATIKA ENEO LA MALAZI.

Ndani ya halmashauri ya wilaya ya singida hasa yalipo makao makuu ya halmashauri(ilongero) hakuna huduma bora za chakula, malazi na huduma za kifedha, eneo hili linapokea na kuhudumia watu zaidi ya mia tano(500) kwa siku ambao wanafika hapa kwa masuala mbalimbali ikiwepo afya katika kituo cha afya na hospitali ya wilaya, shughuli za kisiasa, huduma za mahakama na polisi, shughuli za kibiashara na zaidi ni wageni wanaofika ofisi ya mkurugenzi mtendaji kwaajili ya kupata huduma mbalimbali. Wageni wote hawa wanahitaji kula, kulala, kuburudika, kutumia huduma za kifedha vitu ambavyo ni mahitaji ya msingi lakini vitu hivyo upatikanaji wake ni wa kiwango cha chini sana.

## MATUKIO, FURSA NA MAENEO YA UWEKEZAJI KATIKA PICHA











JARIDA LA

# VIWANDA NA UWEKEZAJI

TOLEO LA MWAKA 2024-2025

LIMEANDALIWA NA;

OFISI YA MKUU WA MKOAA

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
S.L.P. 05 Singida

Kwa maoni na ushauri wasiliana nasi kupitia
Simu. 026 250 2089/2249
Fax: 026 250 2078
E-mail ras@singida.go.tz info.@singidars.go.tz

Endelea kutufuatilia kwenye kurasa zetu.